TUME YA TAIFA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# COSTECH Jarida

ISSN : 1827-7702 | TOLEO LA : 5 | OKTOBA, 2022




# COSTECH yashiriki uzinduzi wa Sahara Sparks

Ukurasa 5



Ukurasa 9

## Wataalamu na Watafiti wanapaswa kuelimisha jamii - Dkt. Seleman Jafo



## Fursa za ndani na nje kwa wabunifu wa Tanzania

Ukurasa 10

*Jarida la COSTECH limechapwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia Barabara ya Ali Hassan Mwinyi Road, Kijitonyama (Sayansi), Jengo la COSTECH, Dar es salaam, Tanzania | Simu: +255 22 2771358 au +255 22 277 4023 | Barua Pepe: dg@costech.or.tz | Tovuti: www.costech.or.tz*

# Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu



**Dkt. Amos Nungu**
**Mkurugenzi Mkuu - COSTECH**

Kwa niaba ya Menejimenti na Wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), napenda kukukaribisha katika Jarida letu la mwezi toleo la mwezi wa Septemba 2022. Jarida hili linaelezea shughuli mbali mbali zinazotekelezwa na COSTECH katika mwezi husika.

Kwa mwezi huu wa Septemba 2022, baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na COSTECH ni pamoja na kuendesha mafunzo ya kujengeana uelewa wa maswala ya Bioteknolojia kwa makatibu wakuu na manaibu katibu wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kusajili na kutoa vibali vya tafiti 101 zitakazofanyika hapa nchini. Shughuli nyingine ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya utafiti na ubunifu inayotekelezwa kwa ufadhili wa COSTECH hapa nchini, Kutoa mafunzo kwa wabunifu na watafiti namna ya kuendeleza kazi zao za ubunifu na utafiti hapa nchini.

Hizo ni baadhi kazi zilizotekelezwa katika mwezi wa Septemba, 2022. Nichukuwe fursa hii kukukaribisha kusoma taarifa mbali mbali kwenye jarida hili na kuomba maoni yako ya namna ya kuboresha jarida hili
Karibu sana.


# Bodi ya Wahariri

**Mwenyekiti**
Samson John Mwela

**Mratibu**
Dkt. Wilbert Bunini Manyilizu

**Mhariri Mkuu**
Bi. Mary Msungu Kigosi

**Mhariri**
Bw.Faisal Abdul Jalil

**Wajumbe**
Bi. Adeline Ajuaye
Bw. Mboyi Wishega
Bw. Emmanuel Girimwa
Bi. Bestina Daniel

**Msanifu**
Gabriel Chowo





Jarida la COSTECH limechapwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi Road, Kijitonyama (Sayansi), Jengo la COSTECH, Dar es salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2771358 au +255 22 277 4023
Barua Pepe: dg@costech.or.tz
Tovuti: www.costech.or.tz

# Watumishi wa Mahakama Kuu Tanzania watembelea studio ya COSTECH

**Dar es Salaam | Oktoba 12, 2022**

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kupitia Kurugenzi ya Menejimenti ya Maarifa (DKM) Ofisi ya Uhusuiano chini ya Studio yake imetembelewa na watumishi 6 wa Mahakama Kuu ya Tanzania tarehe 5 Oktoba, 2022 kwa lengo la kujifunza namna ya kuendesha Studio na mambo mbalimbali yanayohusiana na Studio'



*Watumishi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano wakipata maelezo ya namna ya kuendesha Studio kutoka kwa Afisa Uhusiano wa COSTECH Bw. Faisal Jalil mara baada ya kutembelea Studio ya COSTECH.*

Akizungumza katika ziara hiyo fupi iliyoambatana na Maafisa Uhusiano sita (6) wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mkuu wa Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano, Ndg Artemony Tiganya amesema tumetembelea Studio hizi kwa lengo la kujifunza zaidi kuhusiana na masuala yote ya studio ili na sisi tuweze fanikiwa kuanzisha studio yetu.

“Nashukuru kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama tumepata fursa kama watumishi wa Kitengo cha Habari kutembelea Studio za Tume ya Taifa Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa ajili ya kujifunza uendeshaji na usimamizi wa Studio” alisema Bw. Artemony“ Tumejifunza mambo mengi na tumepata ushirikiano mzuri kutoka kwa watumishi wenzetu tutatumia fursa hii kuanzisha Studio yetu na tutaendelea kushirikiana na Tume, kuhakikisha na sisi tunatoa Elimu na Huduma ya Habari na saa ikilenga jamii kujua haki zao” aliongeza.

Kwa upande wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) Afisa Uhusiano wa COSTECH, Bw. Faisal Abdul alitoa neno la shukrani kwa watumishi wa Mahakama Kuu ya Tanzania kuchagua kutembelea Studio za COSTECH na kuahidi kuendelea kuongeza ushirikiano wa pamoja na wasisite kufika COSTECH pindi itakapohitajika kufanya hivyo.

Watumishi hao walihitimisha ziara hiyo kwa kutembelea Atamizi ya DTBi iliopo chini ya COSTECH inayotumika kulea wabunifu wenye makampuni machanga ikiwemo UJUZI net, Shule Yetu, Iglobal na wengineo.




# Rasimu ya muongozo unaosimamia masuala ya jinsia katika Tafiti na Ubunifu

**Dar es Salaam | Okt 20, 2022**

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imeandaa mkutano wa majadiliano na wadau mbalimbali kuweza kupitia rasimu ya muongozo unaosimamia masuala ya jinsia katika Tafiti na Ubunifu.

Mkutano huo umefunguliwa na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia Dkt. Amos Nungu, na ulifanyika Oktoba 20, 2022 katika ukumbi wa COSTECH uliopo kijitonyama jijini - Dar es salaam.

Dkt. Nungu amesema naishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wakuu wa Taasisi mbalimbali, Wataalamu na wengine wote waliofika na tupo hapa kwaajili ya kushiriki kikao kazi hiki

"Sasa hivi tunafanya kazi na wadau wengi wa maendeleo na tunaona mwenendo unaenda kwenye ushirika badala ya kushughulika na Tanzania wanataka kushughulika na Afrika Mashariki badala ya kushughulika na COSTECH wanataka kushughulika na kundi, sasa kwa muktadha huo angalau kwa Mashariki na Kusini mwa Afrika tumeonekana tupo vizuri katika masuala ya mifumo ya kutoa grants(Mwega) Research na wameambiwa waje kujifunza kwetu kwa sababu tuna mifumo ambayo ina faida chanya kwa Taifa la Tanzania." amesema Dkt. Nungu.

Aliendelea kusema kwenye masuala ya jinsia, Utafiti na Ubunifu kuna mradi unaondelea sasahivi nadhani ukiondoa Afrika Kusini sisi bado tunafanya vizuri, lakini kwa sasa mambo yetu hayapo kwenye kumbukumbu kwahiyo tunavyokaa kwenye vikao kama hivi kujadili na kuchangia inaonekana kwamba Tanzania tupo mbele vizuri zaidi lakini nyaraka hatuna ndio maana tukasema ikiwezekana acha tuendelee kuongozwa. Pia Dkt. Nungu aliongezea kwa kusema sisi kwetu tuna Knowledge Studio, ambayo hutumika kuandaa taarifa mbalimbali za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwasababu leo tuna wataalamu, wadau wakereketwa wa masuala yanayohusiana na jinsia kwenye Utafiti na Ubunifu na changamoto ilipo kwamba ni kwa kiasi gani kuna Ubunifu. hasa tukija kwenye jinsia kuibua hawa wachache waingie huku juu, inafanya tunaonekana hatufanyi vizuri lakini kwa ujumla wake kuna kazi tunafanya ndio maana kuna haja ya kuwa na Wizara maalumu.

Nae Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo jinsia na makundi maalum Bw. Amos Mpanju alisema sisi kama Serikali ya Awamu ya sita tunaheshimu sana masuala ya Utafiti na Ubunifu na hasa zinazolenga kuwa na jicho la kijinsia.

Nimekuja kushiriki mkutano huu na kuchangia maoni yetu na mwisho na nitahitimisha kama mlivyo niheshimisha. Bw. Amos Mpanju "alifafanua kuwa unapoongelea jinsia ni pande zote wake kwa waume,

kwahiyo hamasisho zote ni Utafiti na Ubunifu ambazo zitawajibika kwenye masuala ya jinsia na makundi maalumu, na Serikali yetu ya Awamu ya sita mwelekeo na msisitizo wake ni usawa kwa wote, sasa niseme kwa kuwa tunapata mwongozo wa hizi Tafiti ni jambo jema na nitumie fursa hii kueleza machache mfumo kwa ujumla inathibitisha Katiba, Sheria na Sera lakini pia kuna ahadi za nchi, sisi Taifa tumejikabidhi kupitia Rais wetu ambaye ni champion kwenye kutekeleza jukwaa la kizazi chenye usawa."

Vilevile Bw. Mpanju aliongezea kwamba "tukubali COSTECH mnatoa vibali, hivyo mna mfuko na kuhamasisha Tafiti mbalimbali lakini linapokuja suala la jinsia nitaomba kuwe na uratibu kati ya COSTECH na Wizara ya Sayansi Teknolojia ufundi na Wizara ya Maendeleo ya jamii ili tuone jinsi ya kuwa na matengenezo sahihi ya mfumo, kwa sababu kumekuwa na Tafiti nyingi lakini inasafirishaje kuja kwenye vitendo ili wafanya maamuzi Serikalini na kwenye ngazi mbalimbali tuweze kuhesabu vyote bajeti na mchakato wa kufanya maamuzi lakini kwa hatua zote ili jinsia iweze kukubalika kila sehemu maishani."

Aidha Meneja wa Sayansi za jamii ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) Hildegalda Mushi alihitimisha kwa kusema kwa siku ya leo tulikuwa na mkutano muhimu sana Tume ina utaratibu wa kutengeneza miongozo mbalimbali ya kusimamia masuala ya Utafiti na Ubunifu.

Na Katika tukio hili tumepata nafasi ya kuwa na wadau ambao wameshiriki kujadili rasimu ya muongozo wa kusimamia masuala ya jinsia katika Sayansi Teknolojia na Ubunifu.

Bi Hildegalda alifafanua kuwa "Rasimu hii imetengenezwa kwa ushirikiano na tumeshilikisha wadau mbalimbali kutengeneza rasimu hii ikapelekwa kwenye hatua ya kwanza ya mkutano wa wadau ikajadiliwa na kuonekana inafaa kwenda katika hatua ya pili na hatua ya leo ni hatua ya tatu. Lakini lengo la muongozo wetu si kuangalia wanawake tu lakini pia makundi maalum ambayo yanahitaji kuongezewa msukumo zaidi ili waweze kushiriki katika masuala ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu ili kuleta maendeleo kwa Taifa."

Kwahiyo muongozo wetu unazungumzia maendeleo ya umuhimu wa usawa kwa jinsia pia unatilia mkazo katika ngazi ya Elimu ya Juu na Taasisi za Utafiti, kwamba tunataka wanawake na makundi maalumu yapate wigo mpana zaidi kushiriki kwa kutumia muongozo wetu. Na pia tunaangalia katika utoaji maamuzi kwahiyo tunataka kwa kupitia mwongozo huu tuweze kuchangia uwezo uongozaji wa nafasi za wanawake katika ngazi za kufanya maamuzi na katika Bodi zinazofanya maamuzi ngazi ya Teknolojia na Ubunifu, Taasisi za Elimu ya Juu, Taasisi za Utafiti na Maendeleo kuwepo na ushirikiano zaidi wa wanawake. Amesema Bi. Hildegalda.



*Washiriki wa mkutano wa majadiliano na wadau mbalimbali wakifuatilia mjadala wa kupitia rasimu ya muongozo unaosimamia masuala ya jinsia katika Tafiti na Ubunifu.*

# COSTECH YASHIRIKI UZINDUZI WA SAHARA SPARKS




*Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH Dkt. Amos Nungu akiongea na waandishi wa Habari wakati wa uzinduzi wa kongamano la Sahara Sparks*

**Dar es Salaam | Okt 17, 2022**

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia(COSTECH), imeshiriki uzinduzi wa Kongamano la Sahara Sparks iliyoandaliwa na Sahara Ventures na kuhudhuliwa na wadau mbalimbali wakiwemo COSTECH.

Wadau wengine waliohudhuria kongamano hilo ni UNDP kupitia mradi wa FUNGUO pamoja na Clouds Media group ambapo Uzinduzi huo umefanyika Oktoba 17, 2022 katika ofisi za Sahara Ventures zilizopo victoria– Dar es salaam.

Akizindua kongamano hilo Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Sahara Ventures Jumanne Mtambalike, amesema kampuni hiyo tanzu ya Sahara Sparks ambayo imeandaa kongamano la vijana wabunifu na wote wenye hamasa na masuala ya Teknolojia na Ujasiriamali.

“Kwa takribani miaka saba Sahara Ventures wamekuwa wakiandaa kongamano la Sahara Sparks ambayo imekuwa ikionesha njia ya kuleta vijana pamoja wenye mawazo ya kibunifu na watunga Sera ili kuweza kujadili kwa namna gani Ubunifu,



*Waandishi wa Habari wakichukua taarifa wakati wa uzinduzi wa kongamano la Sahara Sparks.*

Teknolojia na Ujasiriamali vinaweza kuwa chachu ya kuchangia maendeleo ya Taifa la Tanzania, kauli mbiu ya kongamano la mwaka huu ni "Potential unleashed".amesema. Hatahivyo Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia COSTECH, Dkt Amos Nungu, amesema "tupo katika uzinduzi wa Sahara Sparks ambapo COSTECH tunajukumu la kuratibu na kukamilisha masuala ya Sayansi na Teknolojia nchini.

Pia tunajivunia kuwa na miundo mbinu wezeshi na mazingira yanayofanya kazi na vijana wanapata fursa ya kuonekana, kusikika na kubadilishana mawazao na fursa za kwenda kuendeleza mawazo hayo".

Akiongezea Meneja mradi wa Funguo Bw. Joseph Manirakiza, aliendelea kwa kusema tunafurahi kushirikiana na Sahara Sparks na tunaendelea kuunga mkono kwasababu moja ya kazi ya Funguo ni kuwezesha wabunifu na wajasiriamali katika kupata mtaji wa kuendeleza biashara zao, pia kushirikiana na wale wote ambao wako mstari wa mbele kukuza vipaji vya wajasiriamali ili waweze kukua zaidi.




*Picha ya pamoja ya wawakilishi kutoka Sahara Ventures, COSTECH, Clouds Media group na UNDP – Funguo mara baada ya uzinduzi wa kongamano la Sahara Sparks*

# Jamii yaelemishwa madhara ya sumu kuvu

**Kilimanjaro | Oktoba 21, 2022**



*Msimamizi Mkuu wa mradi Prof. Athanasia Matemu (NM – AIST) akitoa utambulisho wa mradi kwa washiriki wa warsha ya kuwasilisha matokea ya Utafiti wa uwepo wa Sumukuvu katika mnyororo wa thamani wa chakula cha ng'ombe na maziwa ilioshirikisha wadau wa Sekta ya wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa kutoka katika Wilaya ya Hai, Mpwapwa na Serengeti iliofanyika Moshi, Kilimanjaro.*

Jamii za wakulima na wafugaji kutoka katika mikoa ya Dodoma, Mara na Kilimanjaro wamepatiwa elimu juu ya namna bora ya kuhifadhi vyakula vya mifugo ili kuwalinda na madhara ya sumukuvu ipatikanayo kwenye mazao ya mifugo iliyokula vyakula vyenye sumu hiyo.

Elimu hiyo ilitolewa katika warsha ya kusambaza matokeo ya utafiti wa mradi wa kuangalia uwepo wa sumukuvu na visababishi vyake katika vyakula vya mifugo na maziwa ya ng'ombe uliofadhiliwa na Tume ya Sayansi na teknolojia (COSTECH), ambapo jumla ya shilingi milioni sabini ilitumika kugharamia mradi huo ambao utekelezaji wake ulikuwa kati ya mwaka 2020 na 2022.

Akizungumza katika warsha hiyo Mtafiti Mkuu wa mradi huo Prof. Athanasia Matemu kutoka Taasisi ya Afrika ya



*Picha ya pamoja ya Watafiti na washiriki wa warsha ya kuwasilisha matokeo ya Utafiti wa uwepo wa Sumukuvu katika mnyororo wa thamani wa chakula cha ng'ombe na maziwa kutoka katika Wilaya ya Hai, Mpwapwa na Serengeti iliofanyika Moshi mkoani Kilimanjaro.*

Sayansi na Teknolojia Nelson Mandela alisema kuwa zaidi ya asilimia 86 ya vyakula vya mifugo vilivyokutwa kwa wafugaji na wauzaji wa vyakula vya mifugo vilikuwa na sumukuvu.

Aidha zaidi ya asilimia 30 ya maziwa yaliyochukuliwa na kupimwa wakati wa utafiti huo yalikutwa na kiwango kikubwa cha sumu kuvu ambacho ni hatari kwa afya ya binadamu. Aliendelea kueleza kuwa wafugaji wengi hawana uelewa wa kutosha juu ya madhara ya sumukuvu na namna bora ya kuhifadhi vyakula vya mifugo ambapo zaidi ya asilimia 74 ya wafugaji katika maeneo yaliyofanyiwa utafiti hawazingatii ukaushaji wa vyakula vya mifugo, jambo ambalo huchangia uwepo wa sumukuvu katika vyakula hivyo.

Alisema mbali na ukaushaji nauhifadhi sahihi wa vyakula vya mifugo ilielezwa kuwa matumizi ya njia bora za kilimo kama vile kupanda na kuvuna kwa wakati, kuweka mbolea na kilimo cha mzunguko yanaweza kupunguza mazingiza wezeshi ya kuenea kwa sumukuvu katika mazao/ vyakula vya mifugo.

Warsha hiyo ya siku moja iliyohusisha wadau mbalimbali wakiwemo wakulima, wafugaji, watengenezaji na wauzaji wa vyakula vya mifugo, viongozi wa Serikali za Mtaa na Maafisa Ugani ilifanyika tarehe 21 Oktoba 2022 katika ukumbi wa mikutano wa Chuo cha Uhamiaji Moshi mkoani Kilimanjaro.

Warsha hiyo ya siku moja iliyohusisha wadau mbalimbali wakiwemo wakulima, wafugaji, watengenezaji na wauzaji wa vyakula vya mifugo, viongozi wa Serikali za Mtaa na Maafisa Ugani ilifanyika tarehe 21 Oktoba 2022 katika ukumbi wa mikutano wa Chuo cha Uhamiaji Moshi mkoani Kilimanjaro.



*Picha ya pamoja ya Watafiti na washiriki wa warsha ya kuwasilisha matokeo ya Utafiti wa uwepo wa Sumukuvu katika mnyororo wa thamani wa chakula cha ng'ombe na maziwa*

# Wataalamu na Watafiti wanapaswa kuelimisha Jamii - Dkt. Jafo

**Dar es salaam | Oktoba, 2022**

Wataalamu na Watafiti wa Bioteknolojia nchini wametakiwa kutoa ushauri wa kisayansi wenye tija kwa Serikali ili kusaidia Taifa kusonga mbele.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira, Dkt. Seleman Jafo, alisema hayo wakati akizindua Mkutano Mkuu wa Chama cha Bioteknolojia Tanzania (BST), jijini Dar es Salaam.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Seleman Jafo mara baada ya uzinduzi wa Chama cha Bioteknolojia Tanzania (BST).*

Jafo alisema katika ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia nchini Tanzania kumekuwepo na mgongano mkubwa wa mawazo, watu wamekuwa na hofu, inawezekana ni hofu ya kisayansi, kutokujua faida zake au ya kibiashara.

Alisema ili kuondoa hofu hiyo, Wataalamu na Watafiti wanapaswa kuelimisha jamii kuhusiana na teknolojia hizo ikiwemo ya Uhandisi Jeni (GMO).

" Watafiti na Wasomi tukikamilisha majawabu ya Teknolojia zilizopo na tukaweka wazi matokeo, watanzania wataelewa," alisema na kuongeza kuwa wataalam wako tayari kushughulikia mambo ya kitafiti na kitaalam nchi isonge mbele. Awali Mwenyekiti wa BST, Profesa Peter Msolla alisema pamoja na nchi kuwa na Sera zinazohimiza matumizi salama na endelevu ya bioteknolojia ya kisasa, na kuwa na mfumo thabiti wa usimamizi; utafiti wa kutumia teknolojia ya GMO katika sekta ya kilimo umesitishwa kutokana na maelekezo ya Wizara husika.

"Vituo vya Utafiti vilivyosimamisha Utafiti vilivyokuwa vikifanya utafiti wa mazao ya mahindi na muhogo. Hii ni changamoto kubwa ambayo inaturudisha nyuma kama Taifa.

"Tunaishauri Serikali kuangalia upya maamuzi hayo kwa sababu bila kufanya utafiti hatuwezi kupata majibu ya maswali yanayoulizwa na wadau mbalimbali kuhusu faida na hasara za bioteknolojia ya kisasa.," alisema.



*Washiriki wakifuatilia mada mbalimbali siku ya uzinduzi wa Chama cha Bioteknolojia Tanzania (BST).*



Wabunifu wakifuatilia mada kuhusu fursa zilizopo ndani na nje kutoka kwa Mtaalam Bw. Lado Kocklekorn

# Fursa za ndani na nje kwa Wabunifu wa Tanzania

Dar es salaam | Okt 29, 2022

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imepokea ujumbe kupitia Wataalamu Waandamizi wa Uholanzi, Bw. Ludo Kocklekorn kwa ajili ya mafunzo mafupi ya siku moja wakishirikiana na Dar Teknohama Business incubator (DTBi).

Dhumuni la mafunzo hayo ni kujifunza na kutengeneza Fursa za ndani na nje kupitia ushirikiano.

Mafunzo hayo yamefanyika ndani ya ofisi za COSTECH na kuhudhuriwa na wajuzi 12 toka DTBi siku ya tarehe 29 Oktoba, 2022 kijitonyama jijini Dar Es Salaam.

Akielezea hayo, Meneja Uendelezaji Biashara (Business Development Manager) Bw. Elia Kinshanga amesema DTBi ikishirikiana na Ujuzi Tanzania Skills Forum imeendesha mafunzo kwa ajili ya kujifunza na kutengeneza fursa za ndani na za nje na kuangalia ni kwa namna gani wanaweza kutengeneza maudhui ili kwenda kuwafundisha wengine. Kwahiyo mafunzo haya yataweza kujenga fursa zaidi kupitia ushirikiano na watu wa nje na itasaidia wao kuja kuwekeza DTBi.

” Dhamira kubwa ya mafunzo haya tukishirikiana na Ujuzi Tanzania skills forum ni kutoa maudhui yao kwa wajuzi wetu wa ndani ili kuangalia namna gani ya kutengeneza fursa mbalimbali za ndani na nje ambayo itasaidia kubadilishana wataalamu na uzoefu pia.



Mtaalamu kutoka Uholanzi akitoa mada kwa wabunifu wa Tanzania

# Hongera Dkt. Wilbert Manyilizu



*Watumishi wa COSTECH wakiwapokea Maharusi Dkt. Wilbert Manyilizu mtumishi wa COSTECH na mkewe Agnes siku ya tarehe 21 Oktoba, 2022 Hekima Garden.*



*Bw. na Bi Wilbert Manyilizu wakiingia ukumbini*



*Kamati ndogo ya maandalizi ya harusi ya Dkt. Wilbert Manyilizu wakipeleka zawadi ya maharusi.*

*15. Wapambe wa maharusi wakiingia ukumbini.*



*Wapambe wa maharusi wakiingia ukumbini.*



*Bi. Sarah Kabigi Mjumbe wa kamati akitoa neno kwa maharusi..*